

Kiolesura cha Mtandao wa Chanjo (VINI)

Jinsi ya Kujisajili kwa Chanjo ya COVID-19 na Mwanakaya

Karatasi hii ya Vidokezi ni kuwasaidia wakazi wa New Hampshire kuratibu miadi ya chanjo ya COVID-19 kwa ajili yao na mwanafamilia katika Kiolesura cha Mtandao wa Chanjo cha New Hampshire (VINI).



Je, ninaweza kumleta mwanakaya kwenye miadi yangu?

Unaruhusiwa kuleta mwanakaya mmoja (1) kwenye miadi yako *ikiwa pia anastahiki katika awamu yoyote iliyo wazi*. Baada ya kujisajili na kuamilisha akaunti yako, sajili mwanakaya wako kwa kubofya kigae cha **Ongeza Mwanafamilia** kwenye VINI. Baada ya kusajili mwanakaya wako, anaweza kuandamana nawe kwenye miadi yako bila kuratibu miadi tofauti.

Tafadhali Kumbuka: Ikiwa unasajili mwanakaya wako kupitia mchakato huu, mawasiliano yote yatatumwa kwa anwani ya barua pepe ambayo ilisajili akaunti katika VINI. Ikiwa mwanakaya wako angependelea kusimamia miadi yake ya chanjo ya COVID-19 na kupokea mawasiliano ya moja kwa moja, tafadhali mwagize akamilishe kwa kujitegemea mchakato wa uchunguzi na usajili kwa kutumia anwani ya barua pepe tofauti na ile iliyotumiwa tayari.

Je, ninaongezaje mwanakaya kwenye akaunti yangu?

- Bofya **Ongeza Mwanafamilia** kwenye ukurasa wa **Kwanza** wa VINI na kisha bofya **Ongeza Mwanafamilia**.
- Utapitishwa mchakato wa uchunguzi na usajili kwa mwanakaya wako.
 - Ikiwa unamsajili mwanakaya, utalazimika kujibu maswali kuhusu historia yake ya matibabu na mzio wowote ambao utaathiri chanjo. Pitia "[Kuna nini katika Chanjo](#)" ya CDC ili kuelewa ikiwa mwanakaya wako anaweza kuwa mzio kwa viambato vyovyote katika chanjo za COVID-19.
- Mara tu wanakaya wote wawili watakaposajiliwa, nenda kwenye **Unda/Simamia Miadi** kwenye ukurasa wa kwanza wa VINI na ufuata hatua za kuratibu miadi yako ya chanjo ya COVID-19. Miadi utakayoratibu itakuwa kwa ajili yako na mwanakaya wako.



Nini cha kukumbuka kuhusu miadi ya mwanakaya wako:

Mara tu utakapomaliza usajili wako na kuongeza mwanafamilia anayestahiki, mwanafamilia wako anashirikiwa kwa miadi yako. Miadi yake ya chanjo sasa imeunganishwa na yako na itabadilika iwapo/wakati miadi yako inabadilika au ukichagua kughairi miadi yako.

Hongera – umewekea nafasi miadi ya chanjo ya COVID-19 kwa ajili yako na mwanakaya!

Iwapo una maswali yoyote katika mchakato huu, tafadhali piga simu 2-1-1 kwa usaidizi.